



## Hakitosimama Kiyama mpaka watu wajifaharishe katika Misikiti

Kutoka kwa Anasi bin Maliki -radhi za Allah ziwe juu yake- Ya kwamba Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Hakitosimama Kiyama mpaka watu wajifaharishe katika Misikiti".

[Sahihi] [Imepokelewa na Abu Daud, Nasai na Ibn Majah]

Anaeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake: Kuwa miongoni mwa dalili za kukaribia kwa Kiyama na kumalizika kwa Dunia, ni watu kujifaharisha kwa kuipamba Misikiti yao, au kujifaharisha kwa dunia yao ndani ya misikiti ambayo haikujengwa ila kwa ajili ya kumtaja Mwenyezi Mungu.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/10897>

النجاة الخيرية  
ALNAJAT CHARITY

